**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

## CHUO CHA MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI

# TAARIFA KWA UMMA: UTEUZI

***Dodoma , Ijumaa Mei 30, 2025.***

Ninapenda kuwataarifu Wanajumuiya wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini na Umma kwa ujumla kuwa, katika Kikao chake cha 141 kilichofanyika leo Ijumaa Mei 30, 2025 pamoja na mambo mengine, Baraza la Uongozi wa Chuo kwa kuzingatia Sheria ya Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Sura 174 Kifungu 9(1) kinachohusu uteuzi, kimewateua watumishi wafuatao kushika nyadhifa mbalimbali za uongozi chuoni kama ifuatavyo : -

1. **Dkt. Fredrick Mfinanga Alleni** ameteuliwa kuwa Mkuu wa Masuala ya Taaluma wa Kituo cha Mafunzo cha Kanda ya Ziwa - Mwanza. Dkt. Alleni anachukua nafasi ya Dkt. Daniel Fabiano Mpeta anaemaliza muda wake;

2. **Dkt. Caroline Geofrey Ngereza** ameteuliwa kuwa Mkuu wa Masuala ya Mipango, Fedha, na Utawala wa Kituo cha Mafunzo cha Kanda ya Ziwa - Mwanza. Dkt. Ngereza anaendelea kipindi cha pili;

3. **Dkt. Edmund Edward Zakayo** ameteuliwa kuwa Mkuu wa Idara ya Mafunzo ya Idadi ya Watu. Dkt. Zakayo anachukua nafasi ya Dkt. Maseke Richard Mgabo ambaye aliteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Taaluma ;

4. **Dkt. Judith Namabira** ameteuliwa kuwa Mkuu wa Idara ya Fedha za Maendeleo na Mafunzo ya Uongozi. Dkt. Namabira anaendelea kipindi cha pili ; na

5. **Dkt. Emmanuel Amitwise Hauli** ameteuliwa kuwa Mkuu wa Kitengo cha Uthibiti Ubora. Dkt. Hauli anachukua nafasi ya Dkt. Christina Geofrey Mandara anaemaliza muda wake.

Viongozi hawa watahudumu katika nafasi hizi kwa muda wa miaka mitatu kuanzia Julai 1, 2025 hadi Juni 30, 2028.

**Imetolewa na,**

Godrick A.Ngolly

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko**